**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**

# HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

**ILIYOWASILISHWA NA**

**MHESHIMIWA RIZIKI PEMBE JUMA (MBM)**

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**

**KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI**

**MEI, 2025**

# YALIYOMO

A.UTANGULIZI..................................................................................1
B.MUUNDO NA MAJUKUMU YA WIZARA YA
MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO.......3
C.UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA
KIPINDI CHA JULAI 2024 – MACHI 2025 ...............................5
Ukusanyaji wa Mapato ..........................................................................5
Mafanikio na Changamoto.....................................................................5
Mapato na Matumizi ..............................................................................7
D.UTEKELEZAJI WA MIRADI NA PROGRAMU
ZINAZOSIMAMIWA NA WIZARA ..........................................8
E.UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA PROGRAMU ZA FUNGU
LA WIZARA.....................................................................................10
Programu ya Hifadhi ya Jamii (PH0401)..........................................11
Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara (PH0402) ..............17
Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji (SH040201) ................17
Programu ndogo ya Uratibu Mipango, Sera na Utafiti (SH040202) 21
Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji Ofisi Kuu
Pemba (SH040203).............................................................................24
Programu ya Maendeleo ya Jamii na Jinsia (PH0403) .....................25
F.MWELEKEO WA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA
2025/2026 .........................................................................................29
Programu ya Hifadhi ya Jamii (PH0401)..........................................33
Programu ya Utawala na Uendeshaji (PH0402) ...............................34
Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji (SH040201) ................34
Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti
(SH040202)........................................................................................35

Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji Ofisi Kuu Pemba (SH040203)....................36
Programu ya Maendeleo ya Jamii na Jinsia (PH0403)....................36
G. SHUKURANI....................37
H. HITIMISHO....................42
Kiambatanisho Nam. 1: Muhtasari wa Upatikanaji wa Fedha kwa Kipindi cha Julai 2024 – Machi 2025....................46
Kiambatanisho Nam. 3: Makaazi ya Wazee Unguja na Pemba........49
Kiambatanisho Nam. 4: Taarifa ya Wazee walio katika Mpango wa Pencheni Jamii....................49
Kiambatanisho Nam. 5: Malalamiko ya Matunzo na Mvutano wa Malezi....................50
Kiambatanisho Nam. 6: Wahanga waliopo Nyumba Salama....................51
Kiambatanisho Nam. 7: Makosa yaliyopelekea watoto kupokewa katika Kituo cha Marekebisho ya Tabia....................51
Kiambatanisho Nam. 8: Vituo Vya Kulelea Watoto Yatima....................52
Kiambatanisho Nam. 9: Vituo vya Malezi na Makuzi ya Awali ya Mtoto....................53
Kiambatanisho 10a: Idadi ya wafanyakazi kwa mujibu wa elimu za.54
Kiambatanisho Nam 10b: Watumishi waliopo masomoni kwa muda mrefu....................55
Kiambatanisho Nam 10c: Watumishi waliopo masomoni kwa muda mfupi....................56
Kiambatanisho Nam. 11: Idadi ya Vikundi na Wajasiriamali kwenye Majukwaa ya Wanawake....................56
Kiambatanisho Nam. 12: Maelezo ya Wizara kwenye bajeti inayozingatia usawa na jinsia....................57

## Vifupishio vya Maneno

| | |
|---|---|
| BAKIZA | Baraza la Kiswahili Zanzibar |
| CCM | Chama Cha Mapinduzi |
| CDC | Shirika la Afya ya Jamii |
| CRDB | Benki ya Maendeleo Vijijini Tanzania |
| CRF | Shirika la Mtandao wa Haki za Watoto Zanzibar |
| C-SEMA | Huduma ya Simu ya Mtoto |
| DPP | Mkurugenzi wa Mashtaka |
| EU | Umoja wa Nchi za Ulaya |
| GEF | Jukwaa la Kizazi chenye Usawa |
| IOM | Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Wahamiaji |
| IPA | Chuo cha Utawala wa Umma |
| ITV | Independent Television |
| JKU | Jeshi la Kujenga Uchumi |
| JUWAZA | Jumuiya ya Wastaafu na Wazee Zanzibar |
| JUYAWAZA | Jumuiya ya Wazee Zanzibar |
| KIU | Kampala International University |
| LSF | Huduma ya Msaada wa Kisheria |
| NBS | Ofisi ya Taifa ya Takwimu Tanzania |
| NMB | Benki ya Taifa ya Biashara Ndogo ndogo |
| NPA-VAWC | Mpango wa Taifa wa Kupinga Ukatili na Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto |
| PBB | Mfumo wa Bajeti unaozingatia Programu |
| PBZ | Benki ya Watu wa Zanzibar |
| PhD | Shahada ya Uzamivu |
| SMT | Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |

| | |
|---|---|
| SMZ | Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar |
| SUZA | Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar |
| TAMWA | Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania |
| TBC | Shirika la Habari Tanzania |
| THESODE | Theatre for Social Development |
| THPS | Tanzania Health Promotion Support |
| TIRA | Mamlaka ya Bima Tanzania |
| TRA | Mamlaka ya Mapato Tanzania |
| UAE | Umoja wa Falme za Kiarabu |
| UNFPA | Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Idadi ya Watu |
| UNICEF | Shirika la Umoja wa Mataifa Watoto |
| UNWOMEN | Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia masuala ya Wanawake |
| USAID | Shirika la Misaada la Marekani |
| UV CCM | Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi |
| UWT | Umoja wa Wanawake Tanzania |
| WHO | Shirika la Afya Duniani |
| ZACA | Jumuiya ya Misaada ya Watoto |
| ZAECA | Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi |
| ZAFELA | Jumuiya ya Wanasheria Wanawake Zanzibar |
| ZAMWASO | Jumuiya ya Misaada ya Wanawake wa Kiislamu |
| ZAPHA+ | Jumuiya ya Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI |

| | |
|---|---|
| ZASO | Jumuiya ya Kusaidia Watoto Yatima na Wanaishi na Virusi vya UKIMWI |
| ZASWA | Jumuiya ya Maafisa ustawi wa jamii Zanzibar |
| ZBC | Shirika la Utangazaji Zanzibar |
| ZC TV | Zanzibar Cable Television |
| ZPC | Shirika la Bandari Zanzibar |
| ZSSF | Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar |
| ZSTC | Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar |
| ZURA | Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar |
| ZU | Chuo Kikuu cha Zanzibar |

## A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha hotuba ya bajeti kwa ajili ya kujadili na hatimaye kuiidhinishia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

2. **Mheshimiwa Spika,** nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujaalia uhai, uzima na afya na kutuwezesha kukutana na kujadili bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

3. **Mheshimiwa Spika,** natoa shukrani za pekee kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuiongoza nchi yetu ikiwa katika hali ya amani na utulivu pamoja na juhudi kubwa anazozichukua katika kuhakikisha jamii ya Wazanzibari inakuwa na ustawi na maendeleo endelevu kupitia uongozi wake wa busara na hekima.

4. **Mheshimiwa Spika,** kipekee naomba kutumia fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa juhudi zake anazozichukua katika kuliongoza taifa letu na kuimarisha usawa wa kijinsia na maendeleo kwa ujumla.

5. **Mheshimiwa Spika,** shukrani za dhati ziende kwa Makamu wa Kwanza wa Rais Mheshimiwa Othman Masoud Othman na Makamu wa Pili wa Rais Mheshimiwa Hemed Suleiman

Abdullah kwa kumsaidia na kumshauri vyema Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika utekelezaji wa majukumu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kutuletea maendeleo makubwa katika nchi yetu.

6. **Mheshimiwa Spika,** kwa moyo wa dhati kabisa naomba kuchukua fursa hii kumpongeza mama yetu mpendwa, mke wa Rais wa Zanzibar, na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Zanzibar Maisha Bora, Mama Mariam Mwinyi, kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto katika kuimarisha ustawi wa wanawake, watoto, wazee na jamii kwa ujumla.

7. **Mheshimiwa Spika,** naomba nikupongeze wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wenyeviti wa Baraza lako tukufu pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati mbali mbali za Baraza kwa umahiri katika uendeshaji na usimamizi wa majukumu ya Baraza hili.

8. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inatambua na kuthamini mchango mkubwa wa Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi inayoongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Sabiha Filfil Thani na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Nassor Salim Ali (Jazira) pamoja na Waheshimiwa Wajumbe na Makatibu wa Kamati kwa namna wanavyoshirikiana nasi katika kutekeleza majukumu yao kwa Wizara yangu, pia nashukuru sana kwa kuyapitia mapendekezo ya bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026 na

kutoa michango ambayo imetuwezesha kuandaa hotuba hii na kuiwasilisha mbele ya Baraza hili tukufu.

## B. MUUNDO NA MAJUKUMU YA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

9. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto katika utekelezaji wa shughuli zake za kawaida zinatekelezwa kupitia Idara nne na Ofisi Kuu Pemba kama ifuatavyo:

    i. Idara ya Ustawi wa Jamii na Wazee;

    ii. Idara ya Uendeshaji na Utumishi;

    iii. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti;

    iv. Idara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto; na

    v. Ofisi Kuu Pemba.

10. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ina majukumu yafuatayo: -

    i. Kuweka mazingira bora ya Ustawi wa Jamii, Watoto, Wazee na kuratibu huduma ya Pencheni Jamii;

    ii. Kuimarisha hifadhi ya wazee na utoaji wa misaada ya kiustawi kwa wananchi wanaoishi katika mazingira magumu zaidi;

    iii. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera, Mipango, Tafiti, Ufuatiliaji na Tathmini ya shughuli za Wizara;

iv. Kusimamia nidhamu, maslahi ya rasilimali watu na nyenzo za utendaji kazi ikiwa ni pamoja na kuhifadhi na kutunza kumbukumbu;

v. Kuimarisha mfumo wa hifadhi ya mtoto na kusimamia haki na wajibu wao; na

vi. Kuimarisha uratibu wa ufikiwaji wa usawa wa kijinsia na kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia.

11. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kama zilivyo taasisi nyengine za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatumia mfumo wa bajeti unaozingatia programu (Program Based Budget - PBB) katika utekelezaji wa mpango kazi wake. Wizara imetekeleza shughuli zake kupitia programu kuu tatu ambazo ni:

i. Programu ya Hifadhi ya Jamii (PH0401)

ii. Programu ya Uratibu na Uendeshaji (PH0402) ambayo ina Programu ndogo zifuatazo: -

Utawala na Uendeshaji (SH040201);

Uratibu wa Sera, Mipango na Utafiti (SH040202); na

Utawala na Uendeshaji Ofisi Kuu Pemba (SH040203)

iii. Programu ya Maendeleo ya Jamii na Jinsia (PH0403)

## C. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2024 – MACHI 2025

*Ukusanyaji wa Mapato*

12. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ilikadiriwa kukusanya kiasi cha shilingi 12,000,000.00 kupitia ukodishaji wa Ukumbi wa Mikutano uliopo Sebleni. Hadi kufikia Machi 2025, hakuna fedha iliyokusanywa kutokana na matengenezo makubwa yaliyokuwa yakifanyika katika ukumbi huo. Matengenezo hayo tayari yamekamilika na kukabidhiwa kwa Wizara tarehe 22 Aprili 2025.

*Mafanikio na Changamoto*

13. **Mheshimiwa Spika,** mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa mpango na bajeti ya Wizara ni kama ifuatavyo: -

    i. Kuzinduliwa kwa Muongozo wa Uanzishaji na Uendeshaji wa Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi na kuundwa kwa majukwaa ya Mikoa (4), Wilaya (8) na Shehia (267).

    ii. Kukamilika na kuzinduliwa kwa Mpango wa Pili wa Kitaifa wa Kupambana na Ukatili na Udhalilishaji dhidi ya Wanawake na Watoto (NPA VAWC II);

    iii. Kuendelea kuratibu Mpango wa Pencheni Jamii ambapo mwaka 2020 kulikuwa na wazee 30,127 na kwa sasa wamefikia wazee 32,096, sawa na ongezeko la wazee 1,969;

iv. Kuongezeka kwa idadi ya wanufaika wa familia zenye mazingira magumu zaidi;

v. Kukamilika kwa utafiti wa Kitaifa wa Kupinga Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji dhidi ya Watoto (Violence Against Children Survey – VACS 2024); na

vi. Kutolewa kwa Vitambulisho 31,271 vya huduma za kijamii kwa wazee wenye umri wa miaka 70 na kuendelea.

**14.** **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha utekelezaji wa Julai 2024 hadi Machi 2025, Wizara imekabiliana na changamoto zifuatazo: -

i. Vitendo vya ukatili na udhalilishaji kwa wanawake na watoto bado vinaendelea kujitokeza katika jamii. Wizara kwa kushirikiana na taasisi na wadau mbalimbali inaendelea kutumia mbinu tofauti kukabiliana na vitendo hivyo.

ii. Uwajibikaji mdogo wa wazazi na familia katika kuwatunza na kuwalea watoto pamoja na wazee wao. Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwemo taasisi za serikali na zisizokuwa za kiserikali, viongozi wa dini, mabaraza ya wazee, mabaraza ya watoto, washirika wa maendeleo na jamii kwa ujumla inaendelea kuweka mikakati mbalimbali inayolenga kutatua changamoto hizo.

iii. Kuwepo kwa idadi kubwa ya familia zenye mazingira magumu zaidi ambazo zinahitaji usaidizi. Wizara inafanya jitihada za kuzifikia familia hizo.

*Mapato na Matumizi*

15. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/25, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ilikadiriwa kutumia shilingi 23,315,462,000 ambapo hadi kufikia Machi 2025, shilingi 8,445,454,923 sawa na asilimia 36 ya makadirio ya mwaka zimepatikana. Fedha za matumizi ya kawaida zilizopangwa ni shilingi 9,959,836,000 zinazohusisha mishahara ni shilingi 3,895,000,000 na shilingi 6,064,836,000 za matumizi mengineyo. Kati ya fedha zilizopatikana Shilingi 3,014,216,007 zilitumika kwa ajili ya mishahara ambayo ni sawa na asilimia 77 ya makadirio ya mishahara na shilingi 2,583,388,052 sawa na asilimia 37 zilitumika kwa matumizi mengineyo. Shilingi 310,186,000 za matumizi mengineyo zilitoka kwa Washirika wa Maendeleo. Fedha za maendeleo zilizopangwa ni shilingi 13,152,260,000 zinazohusisha SMZ ni shilingi 4,500,000,000 na shilingi 8,652,260,000 za Washirika wa Maendeleo.Fedha za maendeleo zilizopatikana ni shilingi 2,847,850,864 sawa na asilimia 21 ya makadirio ya mwaka. Kiambatanisho nambari 1 kinatoa ufafanuzi.

## D. UTEKELEZAJI WA MIRADI NA PROGRAMU ZINAZOSIMAMIWA NA WIZARA

16. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inatekeleza Miradi miwili ambayo ni Mradi wa Hifadhi ya Wazee uliopangwa

kufanya matengenezo majengo ya Wazee ya Sebleni Unguja na Limbani Pemba; na Mradi wa Maliza Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji wa Wanawake na Wasichana unaotekelezwa kwa mashirikiano na UN-WOMEN.

17. **Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Hifadhi ya Wazee ulipangiwa kiasi cha shilingi 4,500,000,000 na hadi kufikia Machi 2025 mradi uliingiziwa shilingi 2,705,200,464 ambayo ni sawa na asilimia 60. Kupitia mradi huu, Wizara imefanya matengenezo makubwa ya majengo ya makaazi ya Wazee Sebleni na Limbani. Majengo mawili na Ukumbi wa mkutano Sebleni yameshakamilika na kukabidhiwa kwa Wizara tarehe 22/4/2025. Kwa upande wa Pemba matengenezo yamefikia asilimia 78 na matarajio ni kukamilika kwa matengenezo hayo ndani ya mwaka wa fedha 2024/2025.

18. **Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Maliza Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji wa Wanawake na Wasichana ulipangiwa kiasi cha shilingi 536,000,000 na hadi kufikia Machi 2025 mradi uliingiziwa shilingi 142,650,400 ambayo ni sawa na asilimia 27. Kupitia mradi huu, Wizara imeandaa na kuzindua Mpangokazi wa Pili wa Kitaifa wa Kupambana na Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto (2025 - 2030) na kuandaa Sera ya Maendeleo ya Jamii ambayo inaendelea kukamilishwa. Aidha, mradi umewawezesha watendaji wa Wizara kushiriki katika mikutano ya kimataifa ya Hali na Hadhi ya Wanawake Duniani (CSW 69), kuadhimisha Siku 16 za Kupinga

Udhalilishaji na Siku ya Wanawake Duniani; na kufanya uratibu wa wadau wanaotekeleza shughuli za mapambano ya Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto.

19. **Mheshimiwa Spika,** mradi wa PAMOJA ulipangwa kutekelezwa kuanzia mwaka wa fedha 2024/2025 na ulitengewa shilingi 8,111,626,000. Hata hivyo, taratibu za kuanza utekelezaji wa mradi huo zilikuwa hazijakamilika ambapo nyaraka za mradi zimetiwa saini mwezi wa Disemba 2024 na matayarisho ya utekelezaji yameendelea hadi tarehe 30/04/2025 ilipotolewa barua ya ithibati ya kuanza utekelezaji wa mradi. Mradi huu unatarajiwa kuanza kutekelezwa rasmi katika mwaka wa fedha 2025/2026.

20. **Mheshimiwa Spika,** Wizara pia inatekeleza Programu ya Kupinga Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto ambayo ilitengewa jumla ya shilingi 208,000,000 na hadi kufikia Machi 2025 programu iliingiziwa shilingi 208,000,000 ikiwa ni sawa na asilimia 100 ambazo zilitumika kufanya tathmini ya vituo vya mkono kwa mkono, kufanya mikutano mitano (Unguja 3 na Pemba 2) ya kupokea maoni kutoka kwa Watu wenye Ulemavu kuchangia Mpango Kazi wa Pili wa Kitaifa wa Kupambana na Udhalilishaji (NPA VAWC II) 2025-2030, na kuendesha jukwaa la mashauriano na wadau wa kupambana na vitendo vya udhalilishaji.

## E. UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA PROGRAMU ZA FUNGU LA WIZARA

21. **Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo sasa naomba uniruhusu kutoa taarifa ya utekelezaji wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kwa kuzingatia malengo yaliyowekwa kupitia programu mbali mbali.

22. **Mheshimiwa Spika,** shughuli zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2024/2025 zilizingatia Sera, Sheria, Mikakati ya Kitaifa na Kimataifa, Ahadi za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Maelekezo ya Serikali pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi - CCM (2020-2025). Katika kipindi cha utekelezaji, Wizara ilijiwekea malengo katika maeneo yafuatayo: -

i. Kuimarisha usimamizi wa shughuli za Wizara ikiwemo kutayarisha na kufanyia mapitio zana za kufanyia kazi za masuala ya maendeleo ya jamii, jinsia, wazee na watoto;

ii. Kuimarisha nguvu kazi na mazingira mazuri ya kazi ikiwemo upatikanaji wa vitendea kazi, matengenezo ya majengo na kuimarisha kumbukumbu muhimu za kiutumishi;

iii. Kuratibu utekelezaji wa sera, tafiti, miongozo, sheria, na kanuni;

iv. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Ahadi za Nchi za Kizazi Chenye Usawa na uwezeshaji wanawake kiuchumi; na

v. Kuimarisha Hifadhi ya Jamii, Wazee, Watoto na Familia zinazoishi katika mazingira magumu zaidi pamoja na kuratibu na kusimamia huduma za Pencheni Jamii.

23. **Mheshimiwa Spika,** naomba nielezee utekelezaji wa kila programu kama ifuatavyo: -

**Programu ya Hifadhi ya Jamii (PH0401)**

24. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina jukumu la kuratibu na kusimamia upatikanaji wa haki kwa makundi yenye mazingira magumu kwa kuimarisha mifumo ya hifadhi ya jamii na huduma kwa wazee, watoto na watu wanaoishi katika mazingira magumu zaidi ili kupunguza kiwango cha umasikini nchini. Shughuli za hifadhi ya jamii zinatekelezwa kwa kuzingatia mikakati ya Kitaifa na Kimataifa, Sheria ya Watoto Nambari 6 ya mwaka 2011, Sheria ya Wazee Nambari 2 ya mwaka 2020 na Sera ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2014. Programu hii ilitengewa shilingi 5,789,835,000 zinazojumuisha shilingi 1,289,835,000 na shilingi 4,500,000,000 za maendeleo. Hadi kufikia Machi 2025 shilingi 3,486,707,639 zilipatikana ikiwa ni sawa na asilimia 60 ya makadirio.

25. **Mheshimiwa Spika,** programu hii ilipanga kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kuendelea kuwahudumia Wazee wanaoishi katika nyumba za Wazee Unguja na Pemba; kuwafuatilia na kuwafikia wazee wanaostahiki kuingia katika Mpango wa Pencheni Jamii na kuwapatia vitambulisho vitakavyowasaidia kupata huduma za jamii;

ii. Kuendelea kufanya matengenezo katika makaazi ya wazee Sebleni na Limbani, kujenga upya makaazi ya wazee ya Welezo na kununua samani kwa ajili ya makaazi hayo; na

iii. Kutoa huduma za hifadhi na ustawi wa jamii kwa watu wenye mazingira magumu zaidi.

**26. Mheshimiwa Spika,** Programu imeendelea kutoa huduma za hifadhi ya jamii kwa kuendelea kuwatunza wazee katika makaazi ya Wazee ya Sebleni, Welezo na Limbani. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya Wazee 67 waliopo katika makaazi ya wazee Welezo 41 (wanawake 13 na wanaume 28), Sebleni 19 (wanawake 13 na wanaume 6) na Limbani wazee saba (wanawake 2 na wanaume 5), wanaendelea kupatiwa huduma za kiustawi ikiwemo chakula, mavazi, malazi, matibabu na fedha za kujikimu. Kiambatanisho nambari 3 kinatoa ufafanuzi.

**27. Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na wadau mbali mbali imeadhimisha Siku ya Wazee Duniani ambayo hufanyika kila ifikapo tarehe 1 Oktoba ya kila mwaka. Maadhimisho hayo kwa mwaka huu yalifanyika tarehe 7 Oktoba 2024 katika Viwanja vya Kufurahishia Watoto

Tibirinzi, Chakechake Pemba ambapo Mgeni Rasmi alikuwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, **Dkt. Hussein Ali Mwinyi.** Kauli mbiu ya mwaka 2024 ilikuwa ni "Kuzeeka kwa Heshima; Umuhimu wa Kuimarisha Matunzo na Mifumo ya Usaidizi wa Wazee Duniani". Aidha, Mabaraza ya Wazee Zanzibar yametoa elimu kuhusu maradhi yasiyoambukiza kwa wazee kupitia redio, televisheni na mikutano ya kijamii kwa lengo la kuwakinga wazee dhidi ya maradhi hayo na kuwashajihisha kutafuta tiba sahihi pale yanapowakuta. Jumla ya vikundi vya mazoezi 65 vimeanzishwa ili kuwachangamsha wazee na kuwajenga kiafya. Vile vile wazee wa mabaraza wameunda vikundi vidogo vidogo 36 vya kujiimarisha kiuchumi na kuanzisha vitalu vya ukulima wa mbogamboga, kutembeleana na kubadilishana uzoefu wa mambo ya kiuchumi na kutatua matatizo yanayowakabili.

28. **Mheshimiwa Spika,** uratibu wa mpango wa Pencheni Jamii kwa wazee waliofikia umri wa miaka 70 na kuendelea umefanyika ambapo jumla ya wazee 32,096 (Unguja 19,130 na Pemba 12,966) wamesajiliwa. Idadi hii inajumuisha wazee wapya 2,883. Katika kipindi hiki pia jumla ya wazee 1,021 wamefariki na kuondolewa katika orodha ya wanufaika wa mpango huu. **Kiambatanisho nambari 4 kinatoa ufafanuzi.**

29. **Mheshimiwa Spika,** katika kuendelea kuimarisha utoaji wa huduma za kiustawi, Wizara imetengeneza vitambulisho vya

wazee 31,271 (Unguja 23,190 na Pemba 8,031). Vitambulisho hivi vinalenga kurahisisha upatikanaji wa huduma zote za kijamii ikiwemo huduma za usafiri, matibabu na msaada kutoka kwa wadau wanaoguswa na huduma za kiustawi. Aidha, vitambulisho vilivyobaki vitaendelea kuchapishwa baada ya Wizara kuhakiki vyema walengwa waliokuwepo kwenye Mpango wa Pencheni Jamii.

30. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ilipokea jumla ya malalamiko 421 yanayohusu ukiukwaji wa haki za watoto na mivutano ya malezi (Unguja 361 na Pemba 60). Malalamiko hayo yamepungua kwa asilimia 61 ukilinganisha na mwaka 2023/2024 ambapo malalamiko yalifikia 691 (Unguja 313 na Pemba 378). Wizara imeendelea kufanyia kazi malalamiko yote yanayopokelewa ili kuhakikisha kuwa haki za watoto zinapatikana kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo. **Kiambatanisho nambari 5 kinatoa ufafanuzi.**

31. **Mheshimiwa Spika,** huduma za Nyumba Salama kwa wahanga wa vitendo vya udhalilishaji na ukatili wa kijinsia zimeendelea kutolewa. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya wahanga watoto 23 walipokelewa kwa ajili ya hifadhi ya muda kutokana na matukio mbali mbali ya udhalilishaji yaliyowakuta (wanawake 13 na wanaume 10). Kiambatanisho nambari 6 kinatoa ufafanuzi.

32. **Mheshimiwa Spika,** Vituo vya Marekebisho ya Tabia kwa watoto wanaokinzana na sheria vilipokea watoto 14 (wanawake 2 na wanaume 12), ambao wamepatiwa

taaluma za stadi za maisha, ushauri nasaha na ufundi stadi. Aidha, ziara za kuwatembelea watoto waliohitimu mafunzo zilifanyika kwa lengo la kuona maendeleo yao. Jumla ya kesi 142 zilifunguliwa Mahakamani (Jinai 59 na Madai 83) ambapo kesi zilizotolewa hukumu ni 12. **Kiambatanisho nambari 7 kinatoa ufafanuzi.**

**33.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea kukisimamia Kituo cha Kulelea Watoto Mazizini chenye jumla ya watoto 26 (wanawake wanane na wanaume 18). Katika kusimamia suala la ulinzi na usalama Wizara imenunua na kufunga kamera za CCTV kwenye Nyumba ya Watoto Mazizini. Aidha, Wizara imefuatilia vituo vya kulelea watoto 16 (Unguja 15 na Pemba kimoja) kwa lengo la kufuatilia huduma zinazotolewa katika vituo hivyo pamoja na kutoa ushauri na maelekezo kwa wasimamizi wa malezi ya watoto. **Kiambatanisho nambari 8 kinatoa ufafanuzi.**

**34.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefuatilia uendeshaji wa vituo 32 (Unguja 22 na Pemba 10) vya Malezi ya kutwa kwa watoto (Day Care Centres). Hatua hiyo ni kwa mujibu wa sheria na taratibu za Serikali. Aidha, taratibu za kuhamasisha uanzishwaji wa vituo zinaendelea ambapo mikutano ya wadau wa vituo vya makuzi na malezi ya awali ya mtoto (ECD) ilifanyika Unguja na Pemba. **Kiambatanisho nambari 9 kinatoa ufafanuzi.**

**35.** **Mheshimiwa Spika,** katika kusimamia mpango wa malezi ya walezi, jumla ya watoto 41 (wanawake 20 na

wanaume 21) wamepatiwa huduma ya malezi na watoto wawili wameunganishwa na familia zao. Aidha, jumla ya walezi wa malezi 189 wamesajiliwa katika Mkoa wa Mjini Magharibi (71), Mkoa wa Kaskazini Unguja (32), Mkoa wa Kusini Pemba (36) na Mkoa wa Kaskazini Pemba (50).

36. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutoa huduma za Ustawi wa Jamii kwa kutoa fedha taslimu kwa familia zenye mazingira magumu zaidi 286 (204 Unguja na 82 Pemba) na kwa akinamama 25 waliojifungua watoto pacha watatu (Unguja 19 na Pemba 6). Aidha, walengwa 44 wanaoishi katika kijiji cha Makundeni pia hupokea huduma hiyo (wanawake 24 na wanaume 20).

37. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea kutoa huduma za mazishi ambapo jumla ya maiti 12 ambazo hazina ndugu zimezikwa na Serikali. Kati ya maiti hizo mbili ni za watoto wachanga.

**Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara (PH0402)**

38. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina jumla ya programu ndogo tatu ambazo ni Utawala na Uendeshaji, Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti; na Utawala na Uendeshaji Ofisi Kuu Pemba. Programu hii ilipangiwa shilingi 15,133,515,000 na hadi kufikia Machi 2025, fedha zilizopatikana ni shilingi 4,133,869,794, sawa na asilimia 27 ya makadirio. Utekelezaji kupitia Programu ndogo hizo ni kama ifuatavyo: -

### *Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji (SH040201)*

39. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ilitengewa shilingi 4,738,047,499 (fedha za mishahara shilingi 3,321,006,264 na shilingi 1,417,041,235 fedha za matumizi mengineyo). Hadi kufika Machi 2025 shilingi 3,304,669,907 (shilingi 2,587,901,370 za mishahara na shilingi 716,768,537 za matumizi mengineyo) zilipatikana ikiwa ni sawa na asilimia 70. Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji ilipanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kuendelea kuwajengea uwezo watumishi wa Wizara na kuwapatia maslahi yao;

ii. Kutekeleza shughuli za uendeshaji wa Ofisi ikiwa ni pamoja na kuipatia Wizara vitendea kazi; na

iii. Kuendelea kuimarisha kumbukumbu na nyenzo nyingine za kiutumishi ili kuweka usimamizi imara wa rasilimali watu katika Wizara.

40. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ilipokea watumishi wapya 13 katika fani ya jinsia, maendeleo ya jamii, utawala na usimamizi wa rasilimali watu. Lengo ni kuongeza ufanisi wa utendaji kazi na kupelekea kuwa na jumla ya watumishi 314 (Unguja 271; wanawake 177 na wanaume 94 na Pemba 43; wanawake 23 na wanaume 20). Pia, Wizara iliwapatia likizo na stahiki zao watumishi 50 (Unguja 38 na Pemba 12) na malipo ya muda baada ya saa za kazi. Aidha, watumishi tisa wamestaafu kazi kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma (6 Unguja na 3 Pemba).

41. **Mheshimiwa Spika,** Wizara katika kuwajengea uwezo watumishi wake inaendelea kuwapatia mafunzo ya muda mrefu watumishi 16 (wanawake 9 na wanaume 7) katika vyuo mbali mbali ndani na nje ya nchi na watumishi 27 (wakiwemo wanawake 14 na wanaume 13) walihudhuria mafunzo ya muda mfupi. Aidha, Wizara ilitoa mafunzo ya kuwajengea uwezo wafanyakazi 260 (wanawake 170 na wanaume 90) juu ya Sheria na Kanuni za Utumishi wa umma, mawasiliano na maadili kwa wafanyakazi, afya ya akili na lishe. Mafunzo hayo yalitolewa kwa mashirikiano baina ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na wataalamu kutoka Ofisi Kuu ya Utumishi, Chuo cha Afya Mbweni na Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma. **Kiambatanisho nambari 10(a,b,c)kinatoa ufafanuzi.**

42. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanya ukaguzi wa ndani kwa nia ya kuimarisha udhibiti wa rasilimali za Serikali. Vile vile, Wizara ilipokea gari mpya nne na kufanya matengenezo ya kawaida ya gari na vyombo vyote vya moto.

43. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha uwajibikaji na utendaji wa Wizara unaimarika jumla ya vikao 18 vilifanyika; Kamati ya Uongozi saba, Kamati Tendaji vitano na vikao viwili vya Kamati ya Ukaguzi. Aidha, vikao vinne vya Bodi ya Zabuni vilifanyika kwa ajili ya kupitia zabuni mbali mbali zilizowasilishwa kulingana na taratibu.

44. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imesaini hati tatu za Makubaliano (MOU) na Chuo cha Maendeleo ya Jamii

Tengeru, Qatar Charity na Zanzibar Maisha Bora Foundation. Mkataba wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru umelenga kuanzisha mashirikiano kwenye maeneo ya Utafiti, mafunzo na ushauri wa kitaalamu. Aidha, mkataba na Zanzibar Maisha Bora Foundation umelenga katika mashirikiano ya kitaalamu na rasilimali watu kwenye kupunguza vitendo vya ukatili na udhalilishaji, uwezeshaji wanawake kupitia vikundi vya wanawake, kushajihisha upatikanaji wa haki za wanawake na watoto pamoja na masuala ya makuzi na lishe. Makubaliano na Qatar Charity yamelenga kusaidia ustawi wa wananchi katika nyanja tofauti.

45. **Mheshimiwa Spika,** matukio mbalimbali yanayohusu Wizara yameripotiwa ambapo habari na picha 96 zilitolewa kwenye mitandao ya kijamii na magazeti yakiwemo Guardian na Zanzibar Leo.

46. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ilishiriki na kupata fursa ya kuhudhuria makongamano na mikutano mbalimbali ikiwemo Mkutano wa 13 wa Afrika Asia Luminary; Kongamano la Wanawake Viongozi la Usafiri wa Anga; Ufunguzi wa Kampeni ya msaada wa kisheria kwa wanawake na makundi maalum; Uwasilishaji wa utekelezaji wa Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa (GEF); Sherehe za miaka 50 za Ubalozi wa Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) na Mkutano wa Mawaziri na viongozi wa juu wa Shirika la Afya Duniani. Mikutano yote hii ilifanyika Jijini Dar es Salaam. Aidha, Wajumbe wa Kamati ya Ustawi wa Baraza la Wawakilishi walipata fursa ya kutembelea kikundi cha

wanawake ambacho ni mfano kwa wajasiriamali wengine katika utekelezaji wa GEF (Newton Group Enterprises) kilichopo Ubungo Dar es Salaam kwa ajili ya kupata mafunzo kwa vitendo kuhusu uwezeshaji wa wanawake.

47. **Mheshimiwa Spika,** katika makongamano na ziara hizo Wizara imeongeza ushirikiano na wadau, wakiwemo Mabalozi wanaoziwakilisha nchi zao kwa kufanya ushawishi wa kushirikiana katika miradi itakayoinua ustawi wa wananchi.

***Programu ndogo ya Uratibu Mipango, Sera na Utafiti (SH040202)***

48. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo hii inashughulikia kuratibu uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa Sera, Miongozo, Mipango ya sekta pamoja na kufanya mapitio ya sheria, kanuni na sera zinazohitaji kufanyiwa marekebisho. Programu ndogo hii ilitengewa shilingi 8,992,763,000 zinajumuisha shilingi 881,137,000 za matumizi mengineyo na shilingi 8,111,626,000 za mradi wa Maendeleo wa PAMOJA unaofadhiliwa na Benki ya Dunia. Hadi kufika Machi 2025, fedha zilizopatikana ni shilingi 136,415,250 ikiwa ni sawa na asilimia 2. Shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kama ifuatavyo: -

i. Kuratibu utayarishaji wa Mipango, Bajeti, na Ripoti za Wizara;

ii. Kuandaa na kuchambua sera zinazosimamiwa na Wizara na Sera nyingine za Kisekta ili kuhakikisha

dhana ya maendeleo ya jamii na mipango na bajeti inayozingatia jinsia zinaendelea kukondoeshwa;

iii. Kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini kwa kuzingatia uratibu wa masuala yote yanayosimamiwa na Wizara; na

iv. Kuratibu utekelezaji wa Miradi.

49. **Mheshimiwa Spika,** tathmini ya majukumu ya Wizara imefanyika, ambayo imeonesha upungufu katika baadhi ya maeneo ya wizara kimuundo na kirasilimali watu. Aidha, imeonesha kuhitajika kwa mashirikiano yanayoratibiwa vyema baina ya Wizara na wadau mbalimbali wakiwemo asasi za kiraia. Kwa ujumla tathmini imeibainishia Wizara haja ya kufanya marekebisho yatakayoimarisha utendaji wake na kuwezesha kufikisha huduma zaidi kwa wananchi.

50. **Mheshimiwa Spika,** Wizara iliwajengea uwezo watendaji watano katika masuala ya ufuatiliaji na tathmini kupitia ushiriki katika Kongamano la Ufuatiliaji, Tathmini na Kujifunza (MEL) na Kongamano la Uwasilishaji wa Matokeo ya Tafiti Barani Afrika. Kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utendaji wa kazi.

51. **Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza maelekezo ya Serikali ya kuzingatia jinsia katika mpango na bajeti ya Serikali, maafisa mipango kutoka wizara 10 walijengewa uwezo pamoja na kuandaa Maelezo ya Kijinsia ya Wizara zao (Ministry Gender Statement). Kati ya Wizara hizo zipo

wizara sita zilizoingia kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na wizara nne zitakazoingia katika utekelezaji wa mwaka wa fedha 2025/2026 (Ofisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji; Wizara ya Maji na Nishati; Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum; na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi). **Kiambatanisho nambari 11 kinatoa ufafanuzi.**

52. **Mheshimiwa Spika,** rasimu ya Sera ya Maendeleo ya Jamii imeandaliwa na ipo katika hatua za kukamilishwa. Sheria ya Watoto Nambari 6 ya Mwaka 2011 inaendelea kufanyiwa kazi ili kuzingatia maagizo yaliyotolewa na Serikali ya kuiimarisha. Aidha, Mradi wa Kukuza Usawa wa Kijinsia (PAMOJA) unaotekelezwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tayari umetiwa saini na kwa sasa matayarisho ya kuanza rasmi utekelezaji wa mradi yanaendelea kufanyika. Hatua zinazoendelea ni kuijengea uwezo Timu ya Usimamizi wa Mradi, wahasibu, Maafisa Ununuzi na Watalamu wa Ufuatiliaji na Tathmini.

***Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji Ofisi Kuu Pemba (SH040203)***

54. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo hii inahusika na uratibu wa masuala yote yanayohusu majukumu ya Sekta ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa upande wa Pemba na ilitengewa shilingi 1,402,704,000 (shilingi 573,994,000 za mshahara na shilingi 828,710,000 za matumizi mengineyo). Hadi kufika Machi 2025 shilingi 692,784,637 (shilingi 426,314,637 za mshahara na shilingi

266,470,000 za matumizi mengineyo) zilipatikana ikiwa ni sawa na asilimia 49 ya pesa zilizopatikana. Shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni hizi zifuatazo:-

i. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Wizara Pemba;

ii. Kuendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa sera, sheria, miongozo na kanuni za Wizara; na

iii. Kuendelea kuwajengea uwezo watumishi, kuweka mazingira mazuri pamoja na kuwapatia maslahi yao.

**55. Mheshimiwa Spika,** Ofisi Kuu Pemba iliratibu ziara za Viongozi wa Wizara kisiwani Pemba pamoja na kushiriki ziara na mikutano mbali mbali ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa wa Serikali. Aidha, ofisi ilifanya ziara za ufuatiliaji katika vikundi vya wajasiriamali wanawake, kituo cha kulelea watoto na Makaazi ya Wazee. Kupitia ziara na mikutano hiyo miongozo, maelekezo na ushauri ulitolewa na kufanyiwa kazi. Vile vile, Ofisi Kuu Pemba imeimarisha upatikanaji wa huduma na vitendea kazi na kuweka mazingira bora ya ofisi.

**Programu ya Maendeleo ya Jamii na Jinsia (PH0403)**

**56. Mheshimiwa Spika,** Programu hii inahusika na jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa haki za Wanawake, Wanaume na Watoto, Programu hii ilitengewa shilingi 2,392,112,000. Hadi kufikia Machi 2025 shilingi 824,877,490 zilipatikana ikiwa ni sawa na asilimia 35.

Aidha, Programu hii inasimamia utekelezaji wa Sera na Sheria zinazohusu Maendeleo ya Jamii kwa kuzingatia Mipango ya Kitaifa, Mikataba ya Kikanda na Kimataifa. Shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kama zifuatazo: -

i. Kuratibu, kusimamia na kutekeleza Mpango Kazi wa Pili wa Kitaifa wa Kupambana na Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto (NPA-VAWC II 2025-2030);

ii. Kuandaa Sera ya Maendeleo ya Jamii pamoja na miongozo ya utoaji wa huduma za maendeleo ya jamii na kukamilisha tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Jinsia;

iii. Kuratibu na kuhamasisha utekelezaji wa Ahadi za Nchi juu ya Kizazi Chenye Usawa;

iv. Kuratibu, kuwawezesha na kuwaunganisha wanawake na fursa mbali mbali;

v. Kuratibu, kuwezesha na kuimarisha mabaraza ya watoto katika ngazi zote; na

vi. Kuhamasisha na kuimarisha malezi ya pamoja.

57. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imekamilisha na kuzindua rasmi Mpango Kazi wa Pili wa Kitaifa wa Kupambana na Ukatili na Udhalilishaji dhidi ya Wanawake na Watoto (NPA VAWC II) 2025-2030 ambao ulizinduliwa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza

la Mapinduzi **Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi.** Mpango huo utaongoza utekelezaji wa shughuli za kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji kwa taasisi za Serikali, Asasi za Kiraia na wadau wengine. Aidha, Wizara iliandaa na kutekeleza Kampeni ya Kupinga Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji "Mtoto Mboni Yangu". Kampeni hii ililenga kuhamasisha jamii kuwalinda Watoto na ilizinduliwa na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, **Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdullah.**

58. **Mheshimiwa Spika,** kuelekea kilele cha Siku ya Wanawake Duniani kulifanyika mikutano ya kuwajengea uwezo wajasiriamali Wanawake (90) Unguja na Pemba na kufanya maonesho ya Wajasiriamali wanawake 100 kutoka mikoa yote mitatu ya Unguja. Lengo ni kuwaleta wanawake pamoja kwa ajili ya kuwahamasisha na kuendeleza juhudi za kujiimarisha kiuchumi pamoja na kutambua haki zao kwa mujibu wa sheria. Maadhimisho hayo yalifanyika katika Viwanja vya Nyamanzi, Mkoa wa Mjini Magharibi ambapo zaidi ya wanawake 10,000 walihamasika na kuhudhuria. Mgeni rasmi alikuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi na kauli mbiu ilikuwa "Ushiriki wa Mwanamke na Msichana ni Kichocheo cha Maendeleo".

59. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imesimamia uanzishwaji wa Majukwaa 279 ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi ambapo majukwaa 267 yameanzishwa katika ngazi ya Shehia, majukwaa manane ngazi ya Wilaya na manne

ngazi ya Mkoa. Jumla ya Vikundi 3,571 (Unguja 1,750 na Pemba 1,821) vyenye wajasiriamali 39,398 (Unguja 17,669 na Pemba 21,729) vilishiriki katika uanzishaji huo wa majukwaa. **Kiambatanisho nambari 12 kinatoa ufafanuzi.**

60. **Mheshimiwa spika,** Wizara iliwapatia mafunzo vijana wa kike 120 kutoka wilaya zote (Unguja 80 na Pemba 40) katika Chuo cha Furahika kilichopo Dar-Es-Salaam katika fani mbalimbali ikiwemo ushoni, upambaji, bandari, ukatibu muhtasi, uhudumu wa hoteli na utalii. Lengo ni kuwapa ujuzi ili waweze kujiajiri wenyewe kupitia fani hizo.

61. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Mipango ilifanya kikao cha kupokea maoni ya watoto kuhusu Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050 kilichowashirikisha watoto 100 kutoka Wilaya zote za Unguja na Pemba. Aidha, Wizara iliyajengea uwezo Mabaraza ya watoto kuhusiana na haki na wajibu wa watoto na namna ya kujikinga na vitendo vya ukatili na udhalilishaji. Watoto 564 (wanawake 303 na Wanaume 261) walishiriki katika mafunzo hayo.

62. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na Jukwaa la Haki za Watoto Zanzibar (ZCRF) imefanya mikutano miwili ya ushawishi na utetezi kwa viongozi wa wilaya. Aidha, Asasi za Kiraia (AZAKI) zinazoshughulika na Watoto zilijengewa uwezo kuhusu bajeti za Serikali na ufuatiliaji wa matumizi

ya Fedha za Umma Unguja na Pemba ambapo jumla ya AZAKI 33 zilishiriki.

63. **Mheshimiwa Spika,** Utafiti wa Udhalilishaji Dhidi ya Watoto na Vijana, uliofanyika Tanzania nzima (Violence Against Children Survey – VACS 2024) umekamilika na hatua zinazoendelea ni kutoa matokeo ya utafiti huo mwezi wa Mei 2025.

64. **Mheshimiwa Spika,** Wizara iliendelea kuelimisha na kuhamasisha jamii juu ya kujikinga na kuripoti matukio ya Ukatili na Udhalilishaji kwa kupitia vyombo vya habari mbalimbali. Jumla ya vipindi 76 vilirushwa hewani kupitia ZBC Redio, ZBC TV, Zanzibar Cable TV, Bahari FM redio, Assalam redio, pamoja na makala 9 kupitia gazeti la Zanzibar Leo. Aidha, Shirika la C-sema, limeendelea kutoa fursa kwa wananchi ya kutoa taarifa zinazohusu matukio ya ukatili kupitia namba 116 bila ya kutozwa kiasi chochote cha fedha.

## F. MWELEKEO WA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2025/2026

### a. Malengo ya Wizara kwa mwaka 2025/2026

65. **Mheshimiwa Spika,** mwelekeo wa utekelezaji wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka wa fedha 2025/2026 umezingatia maelekezo yaliyotolewa na Serikali ya Awamu ya Nane katika kuimarisha utoaji wa huduma. Wizara itahakikisha kwamba

huduma zinaendelea kuimarishwa pamoja na kutia nguvu zaidi kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia na kustawisha jamii. Kwa muktadha huo, vipaumbele vya Wizara vinagusa maeneo yafuatayo: -

i. Kukuza utekelezaji wa Mipango na Mikakati mbalimbali ya Wizara ikiwemo Mpango wa Pili wa Kitaifa wa Kupambana na Ukatili na Udhalilishaji dhidi ya Wanawake na Watoto (NPA VAWC II 2025 - 2030); Mpango wa Pili wa Utekelezaji wa Sera ya Hifadhi ya Jamii; na mikakati ya kuwawezesha wanawake kiuchumi, kisiasa na kijamii ikiwemo kufanyiakazi mpango wa utekelezaji wa Ahadi za Nchi za Kizazi Chenye Usawa GEF) pamoja na Majukwaa ya Uwezeshaji wa Wanawake Kiuchumi;

ii. Kutayarisha na kutekeleza Mpango wa Utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Jamii, kukamilisha mapitio ya Sera ya Jinsia na kukamilisha Sheria mpya ya Watoto;

iii. Kuwahamasisha wanawake katika kushiriki kugombea nafasi za uongozi;

iv. Kuimarisha Huduma za malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto katika ngazi za familia, jamii na taasisi;

v. Kutekeleza Mapendekezo ya Utafiti wa Ukatili na Udhalilishaji dhidi ya Watoto na Vijana (VACS 2024) na tafiti nyingine zinazogusa makundi yanayosimamiwa na Wizara;

vi. Kuimarisha Hifadhi ya Jamii, Wazee, Watoto na Familia zinazoishi katika mazingira magumu zaidi, pamoja na kusimamia Pencheni Jamii na Mabaraza ya Wazee;

vii. Kuratibu utoaji wa huduma za msingi kwa watu wenye mahitaji maalum ikiwemo huduma za msaada wa kisaikolojia kwa manusura wa majanga mbalimbali na makundi mengine yenye uhitaji katika jamii;

viii. Kuimarisha mifumo ya malezi, ulinzi na maendeleo ya watoto na familia.

ix. Kuimarisha uratibu na usimamizi wa Kada za Ustawi na Maendeleo ya Jamii likiwemo suala la kutayarisha Sheria ya Ustawi wa Jamii;

x. Kuratibu Mipango na bajeti inayozingatia Usawa wa Kijinsia katika Wizara, Taasisi, Mikoa na Wilaya; na

xi. Kuimarisha nguvu kazi na mazingira ya kazi ikiwemo upatikanaji wa vitendea kazi, matengenezo ya majengo na kumbukumbu muhimu za kiutumishi.

**b. Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka 2025/2026**

**66.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imekadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 15,000,000.00 kuchangia mfuko Mkuu wa Serikali.

### c. Mwelekeo wa Matumizi kwa Programu

67. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara imekadiriwa kutumia jumla ya shilingi 17,072,042,000. Kati ya fedha hizo shilingi 10,581,521,000 ni za Matumizi ya kawaida, zinazohusisha Mishahara shilingi 4,196,100,000 na shilingi 6,012,021,000 ni za matumizi mengineyo na shilingi 373,400,000 za Ruzuku; na shilingi 6,490,521,000 za maendeleo zinazohusisha shilingi 1,500,000,000 kutoka SMZ na shilingi 4,990,521,000 zinazotoka kwa Washirika wa Maendeleo. **Kiambatanisho Nambari 2 kwa ufafanuzi zaidi.**

### d. Miradi na Programu za Maendeleo

68. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto itatekeleza miradi na programu kama ifuatavyo:-

i. Kuendelea na matengenezo ya majengo matatu ya Sebleni na kukamilisha ujenzi wa nyumba za Wazee Welezo;

ii. Kuendelea kutekeleza Mapambano Dhidi ya Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto kupitia Mradi wa Tokomeza unaotekelezwa kwa ushirikiano na UN Women na Programu inayotekelezwa kupitia UNFPA;

iii. Kusimamia utekelezaji wa Mradi wa Kukuza Usawa wa Kijinsia Tanzania (PAMOJA). Mradi huu unahusisha maeneo makuu manne ya kiutekelezaji ambayo ni:

(a) Kuwawezesha wanawake kiuchumi kwa kuwapatia mikopo itakayosimamiwa na Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (ZEEA);

(b) Kupinga na kukabiliana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia ambapo shughuli kuu ni kujenga Nyumba Salama 2 na Kituo kimoja cha huduma za Kisaikolojia;

(c) Eneo la Ubunifu na Ushirikishwaji linalohusika na ujenzi wa Vituo 16 vya Malezi na Makuzi ya Awali ya Watoto Unguja na Pemba; na

(d) Usimamizi na Uratibu wa Mradi.

**Programu ya Hifadhi ya Jamii (PH0401)**

**69.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara imepanga kutumia shilingi 3,643,223,000 sawa na asilimia 21 ya bajeti ya Wizara kupitia Programu hii kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kuendelea kutoa huduma za kiustawi kwa Wazee ikiwemo kufanyia kazi upatikanaji na matumizi ya vitambulisho na kuimarisha mabaraza ya wazee katika maeneo yao ya makaazi;

ii. Kuendelea na awamu ya pili ya matengenezo katika makaazi ya wazee Sebleni na kujenga makaazi ya wazee ya Welezo; na

iii. Kutoa huduma za hifadhi na ustawi wa jamii kwa watu wenye mazingira magumu zaidi.

iv. Kuimarisha huduma za Malezi na msaada wa Kisaikolojia pamoja na kujenga uwezo wa watoa huduma wa msaada wa Kisakolojia.

**Programu ya Utawala na Uendeshaji (PH0402)**

**70.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara imepanga kutumia shilingi 7,691,816,000 sawa na asilimia 45 ya bajeti ya Wizara.

***Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji (SH040201)***

**71.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara imepanga kutumia shilingi 5,553,920,000 zikiwemo shilingi 3,590,405,000 za mishahara na shilingi 1,963,515,000 za matumizi mengineyo kwa Programu Ndogo hii sawa na asilimia 33 kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kuendelea kuwajengea uwezo watumishi wa Wizara na kuwapatia haki na stahiki zao;

ii. Kutekeleza shughuli za uendeshaji wa Ofisi ikiwa ni pamoja na kuipatia Wizara vitendea kazi; na

iii. Kuendelea kuimarisha kumbukumbu na nyenzo nyingine za kiutumishi ili kuweka usimamizi imara wa rasilimali watu katika Wizara.

***Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti (SH040202)***

**72. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Programu Ndogo hii imepanga kutumia shilingi 432,100,000 za matumizi mengineyo sawa na asilimia 3. Shughuli zilizopangwa ni kama zifuatazo:

i. Kuratibu utayarishaji wa Mipango, Bajeti, na Ripoti za Wizara;

ii. Kuandaa na kuchambua sera zinazosimamiwa na Wizara na Sera nyingine za Kisekta ili kuhakikisha dhana ya maendeleo ya jamii, mipango na bajeti inayozingatia jinsia zinaendelea kukondoishwa; na

iii. Kuendelea kuratibu ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Wizara na kutekeleza mikakati ya kufanyia kazi tafiti za kijamii.

***Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji Ofisi Kuu Pemba (SH040203)***

**73. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara imepanga kutumia shilingi 1,705,795,000 sawa na asilimia 10 ya bajeti ya Wizara zikiwemo shilingi 605,695,000 za mishahara na shilingi 1,100,100,000 za matumizi mengineyo. Kupitia programu ndogo hii, yafuatayo yamepangwa kutekelezwa: -

i. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za kawaida za Wizara Pemba ikiwemo shughuli zinazohusu Ustawi na Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto;

ii. Kuendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa sera, sheria, miongozo na kanuni za Wizara; na

iii. Kuwajengea uwezo watumishi, kuweka mazingira mazuri ya kazi pamoja na kuhakikisha haki na stahiki zao.

**Programu ya Maendeleo ya Jamii na Jinsia (PH0403)**

**74. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara imepanga kutumia shilingi 5,737,003,000 sawa na asilimia 34 ya bajeti ya Wizara. Programu ya Maendeleo ya Jamii na Jinsia imepanga kutekeleza yafuatayo: -

i. Kuyafikia Majukwaa yote ya uwezeshaji wanawake kiuchumi kuanzia ngazi ya Shehia hadi Mikoa;

ii. Kuendelea kuwajengea uwezo wanawake kuweza kuchukua fursa mbalimbali zikiwemo za kiuchumi, kisiasa na kijamii;

iii. Kuhamasisha Wanawake kushiriki kugombea nafasi za uongozi katika ngazi mbali mbali;

iv. Kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Kitaifa wa Kumaliza Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji dhidi ya Wanawake na Watoto (NPA VAWC II), GEF, Mpango wa He for She na Mradi wa Mapambano dhidi ya Vitendo vya Ukatili wa Kijinsia kwa Wanawake na Wasichana; na

v. Kuadhimisha siku za kimataifa na kikanda.

## G. SHUKURANI

**75. Mheshimiwa Spika,** mashirikiano mazuri na Taasisi za Serikali na zisizo za Serikali, mashirika ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa, Sekta binafsi na mtu mmoja mmoja ndio chachu ya mafanikio yaliyofikiwa na Wizara. Kwa niaba ya Serikali, Wizara inatambua na kuthamini michango yao wanayoitoa katika kufanikisha malengo ya Wizara na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ujumla. Wizara hii inasimamia masuala mtambuka kwa Wizara zote na ni dhahiri kuwa dhana nzima ya utoaji wa huduma na maendeleo ya jamii, kulinda ustawi wa jamii (wanawake, wanaume, vijana, wazee na watoto) pamoja na kupinga na kupambana na vitendo vyote vya ukatili na udhalilishaji dhidi ya wanawake na watoto vinahitaji nguvu za pamoja. Kwa niaba ya Wizara natoa shukrani za dhati kwa wote walioshirikiana nasi katika utekelezaji wa shughuli kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**76. Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa shukrani za pekee kwa chama changu, Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa ngazi zake zote na Jumuiya zake (UWT, UVCCM na WAZAZI) kwa kusimamia vyema utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 – 2025. Aidha, ninazishukuru Wizara zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mashirikiano yao waliyoipatia Wizara yangu katika mwaka wa fedha 2024/2025. Nap¬¬¬¬¬enda kuishukuru Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mashirikiano wanayotupatia pamoja na Ofisi ya Makamu

wa Rais na Wizara mbali mbali za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninaishukuru kwa dhati jumuiya ya wanawake Tanzania (UWT) na Kamati ya Kitaifa ya Mapambano ya Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia ya UWT.

**77.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu inatoa shukrani kwa Washirika wa Maendeleo na Mashirika ya Kimataifa kama ifuatavyo: - Ofisi za Ubalozi Mdogo wa China uliopo Zanzibar, Umoja wa Falme za Kiarabu - UAE, Umoja wa Ulaya - EU, Qatar Foundation, World Bank, UNICEF, UNFPA, UNWOMEN, UNESCO, WHO, HelpAge International, SOS, IOM, USAID, Save the Children na CDC. Ninazishukuru taasisi mbalimbali za SMZ na SMT zikiwemo Benki Kuu ya Tanzania, Benki ya Watu wa Zanzibar - PBZ, NMB, CRDB, Benki ya AZANIA, ZURA, Mamlaka ya Mapato Tanzania - TRA, Mamlaka ya Mapato Zanzibar - ZRA, TIRA, Shirika la Bandari Zanzibar - ZPC, Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, ZEEA, SUZA, ZU, Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru na Chuo Kikuu cha SUMAIT.

**78.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu pia imeshirikiana na Taasisi za Sheria ikiwemo Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Mahakama, Jeshi la Polisi na ZAECA. Ninatambua pia mchango wa taasisi ya LSF, Action Aid, Pathfinder, THPS, Step Up Foundation, Nuru Foundation, Noah Foundation and Good People, Mabaraza ya Wazee, JUWAZA, JUYAWAZA, TAMWA, C-Sema, ZASWA, CRF, ZAMWASO, ZASO, ZACA, ZAPHA+, BAKIZA,

Park Hayatt Hotel, THESODE, Zanzibar Maisha Bora Foundation, Mwanamke Initiative Foundation, Daraja Foundation, Asma Mwinyi Foundation, Assalam Foundation, Sino Youth Africa, Taasisi ya Ndoto Ajira, Care Tanzania, Chuo cha Afya Zanzibar, Community Forest Pemba na Zanzibar Vijana Vision Group.

79. **Mheshimiwa Spika,** shukurani za pekee kwa Waandishi wa Habari, Vikosi vya Ulinzi na Usalama vya SMT na SMZ vikiwemo JKU, Uhamiaji (Zanzibar), Mrajis wa NGO's Zanzibar na Wakuu wa Mikoa, Wilaya, Madiwani na Masheha wote wa Shehia 388 za Zanzibar. Ninawashukuru Timu ya kusaidia Mapambano dhidi ya Ukatili na Udhalilishaji wakiwemo; Waratibu wa Wanawake na Watoto wa Shehia, Viongozi wa Dini, Masheha, Timu za Wanaharakati, Wasaidizi wa Sheria, Vituo vya Mkono kwa Mkono pamoja na Timu ya Wanaume wa Mabadiliko. Hakika wao ni kiunganishi muhimu baina ya Wizara na Wananchi katika maeneo mbalimbali. Aidha, natumia fursa hii kuwashukuru wale wote ambao sikuweza kuwataja katika taarifa hii na naomba watambue kuwa mchango wao una thamani sana.

80. **Mheshimiwa Spika,** natoa shukrani za dhati kwa Uongozi na Watumishi wote wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mashirikiano wanayoendelea kunipatia. Ninamshukuru Naibu Waziri, Mheshimiwa Anna Athanas Paul. Hakika ananipa ushirikiano mkubwa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Ninamshukuru

Katibu Mkuu, Ndugu Abeida Rashid Abdallah na Naibu Katibu Mkuu Ndugu Khatib Mwadini Khatib, ambao kwa hakika wanafanya kazi kubwa ya kuiongoza Wizara yetu kiutendaji. Natambua mchango wa Afisa Mdhamini, Ndugu Hafidh Ali Mohamed Shoka na Wakurugenzi wetu wote na naomba niwatambue, Ndugu Hassan Ibrahim Suleiman, Ndugu Siti Abas Ali, Ndugu Daima Mkalimoto na Dkt. Salum Rashid. Natoa shukrani za dhati kwa Wakuu wa Divisheni, Wakuu wa Vitengo, Madereva pamoja na watumishi wote wa Wizara kwa ujumla. Mchango wao ni muhimu katika uhai na ustawi wa Wizara yetu.

**81.** **Mheshimiwa Spika,** naomba nimalizie kwa kuishukuru familia yangu yote kwa kunivumilia na kuniunga mkono katika kutekeleza majukumu yangu ya kila siku ya kiuongozi katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Mwenyezi Mungu awazidishie moyo wa ustahamilivu na kheri nyingi, **Amin.**

**82.** **Mheshimiwa Spika,** nachukuwa fursa hii kuwatakia Watanzania wote uchaguzi wenye Amani na Utulivu ili ipatikane Serikali mpya baada ya Uchaguzi Mkuu unaotegemewa kufanyika mwezi wa Oktoba mwaka huu.

**83.** **Mheshimiwa Spika,** mwisho si kwa umuhimu, napenda kuwashukuru wanawake wenzangu wote wa Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa ushirikiano wao mkubwa walionipatia katika kutekeleza majukumu yangu niliyopewa. Nawaombea kwa Mwenyezi Mungu awazidishie kila lililo

na kheri nao na nawaomba waendelee kuniunga mkono kwa maslahi mapana ya wanawake wa mkoa wetu. Naushukuru uongozi wote wa UWT Mkoa Kaskazini Unguja kuanzia ngazi ya mkoa, wilaya, jimbo, wadi na matawi yote. Naomba niwaahidi kwamba nitaendelea kushirikiana nao siku zote ili kuhakikisha mwanamke wa Kaskazini anasimama imara katika hali zote.


## H. HITIMISHO

**84.** **Mheshimiwa Spika,** naomba nimalizie kwa kufanya marejeo ya maeneo ambayo Wizara yangu inayasimamia. **Maendeleo ya Jamii** ni nguzo muhimu ya kuleta maendeleo katika nchi yetu na kuimarisha misingi ya kuwawezesha watu katika jamii kuwa ndio msingi na wanufaika wa maendeleo. Katika kuwezesha dhamira ya maendeleo inafikiwa, Viongozi wetu wamekuja na ubunifu wa kumuweka mwanamke katika kupata fursa za kujiendeleza kiuchumi kupitia Majukwaa ya Uwezeshaji. Mbali na kumuweka mwanamke katika nafasi ya kipekee, Wizara hii inasimamia haki mtambuka za mtoto ambaye ndiyo nguzo ya taifa letu. Malezi bora ya mtoto, lishe bora, elimu bora na makuzi yenye stara kulingana na mila na silka za Kizanzibari ndiyo lengo letu. Jukumu hili linafanywa kupitia sekta mbali mbali na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ndiyo yenye zana za msingi za kusimamia na kuhakikisha kuwa mtoto wa kizanzibari anaishi katika mazingira bora yatakayompelekea kuwa baba na mama bora wa baadaye.

85. **Mheshimiwa Spika,** sambamba na majukumu haya, Wizara hii inasimamia matunzo kwa wazee wetu ambao wameitumikia nchi hii kwa upendo mkubwa wakati wakiwa vijana katika nyanja mbali mbali. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inaendelea kuwatayarishia vitambulisho Wazee wetu ili waweze kupata huduma bora katika vyombo vya usafiri wa umma, huduma za afya na kwengineko. Masuala haya yanayosimamiwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto yanatuhusu sote hivyo ni wajibu wetu kuitikia wito wa kujenga kizazi chenye usawa kwa kuzingatia namna tunavyoweka mazingira wezeshi kwa wanawake na wanaume kujenga uchumi imara zaidi kwao binafsi, familia zao na hata taifa kwa ujumla. Tafiti zimebainisha kuwa nchi zinazozingatia usawa wa kijinsia zimeweza kuimarika kiuchumi kwa kasi kuliko nchi ambazo hazizingatii usawa huo.

86. **Mheshimiwa Spika,** naomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu waichangie hotuba hii, watushauri ipasavyo na hatimaye waiidhinishie Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto matumizi ya shilingi 17,072,042,000 ili kutekeleza kazi za kawaida na kazi za maendeleo kwa mwaka wa fedha 2025/2026, kwa mchanganuo uliotolewa. Aidha, Mheshimiwa Spika, naliomba Baraza lako tukufu liikubalie Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ichangie kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali jumla ya shilingi 15,000,000.

**87. Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.



…………………………….

**RIZIKI PEMBE JUMA (MBM) WAZIRI**

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**

**ZANZIBAR**

**Kiambatanisho Nam. 1: Muhtasari wa Upatikanaji wa Fedha kwa Kipindi cha Julai 2024 – Machi 2025**

| | | Fedha Zilizopangwa kwa Mwaka | | | Fedha Zilizopatikana | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Program** | **Jumla** | **Mishahara** | **Matumizi Mengineyo** | **Miradi** | **Jumla** | **Mishahara** | **Matumizi Mengineyo** | **Miradi** | **%** |
| Programu ya Utawala na Uendeshaji | 15,133,514 | 3,895,000 | 3,126,888 | 8,111,626 | 4,133,870 | 3,014,216 | 1,119,653 | - | **27** |
| Programu ndogo utawala na uendeshaji | 4,738,047 | 3,321,006 | 1,417,041 | | 3,304,670 | 2,587,901 | 716,768 | | **70** |
| Programu ndogo ya Mipango Sera na Utafiti | 8,992,763 | | 881,137 | 8,111,626 | 136,415 | | 136,415 | | **2** |
| Ofisi Kuu Pemba | 1,402,704 | 573,994 | 828,710 | | 692,784 | 426,314,637 | 266,470 | | **49** |
| Programu ya Hifadhi ya Jamii | 5,789,835 | | 1,289,835 | 4,500,000 | 3,486,707 | | 781,507 | 2,705,200 | **60** |
| Programu ya Maendeleo ya Jamii na Jinsia | 2,392,112 | | 1,648,112 | 744,000 | 824,877 | | 474,227 | 350,650 | **34** |
| **Jumla Kuu** | **23,315,461** | **7,790,000** | **6,064,835** | **22,007,886** | **8,445,455** | **3,014,216** | **2,375,388** | **3,055,851** | **36** |

Chanzo: WMJJWW, 2024/25

**Tanbihi:**

1. Programu ya Utawala na Uendeshaji: Matumizi ya Mradi ni Mkopo kutoka Benki ya Dunia (Makadirio ni Shilingi 8,111,626,000)

2. Programu ya Hifadhi ya Jamii: Matumizi ya Mradi ni fedha za SMZ (Makadirio ni Shilingi 4,500,000,000)

3. Programu ya Maendeleo ya Jamii: Matumizi ya Mradi ni fedha za Ruzuku kutoka UNICEF na UN-WOMEN (Makadirio ni Shilingi 744,000,000)

.. Kiambatanisho Nam. 2: Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka 2025/2026

| Fungu/Idara | Kazi za Kawaida | | | | Kazi za Maendeleo | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Jumla Kuu | Mishahara na Stahiki | Matumizi Mengineyo | Matumizi ya Kawaida | SMZ | Wahisani | | | Jumla Maendeleo |
| | | | | | | UNWOMEN | WB | UNFPA | |
| PH0401 Hifadhi ya Jamii | 3,643,223 | | 1,980,934 | 162,289 | 1,500,000 | | | | 1,500,000 |
| | | | | | | | | | |
| PH0402 Utawala na Uendeshaji | 7,691,815 | 4,196,100 | 3,495,715 | | | | | | |
| SH040201 Utawala na Uendeshaji | 5,553,920 | 3,590,405 | 1,963,515 | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| SH040202 Mipango Sera na Utafiti | 432,100 | | 432,100 | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| SH040203 Utawala na Uendeshaji Afisi Kuu Pemba | 1,705,795 | 605,695 | 1,100,100 | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| PH0403 Maendeleo ya Jamii na Jinsia | 5,737,003 | | 746,482 | | | 555,000 | 4,354,200 | 81,321 | 4,990,521 |
| | | | | | | | | | |
| **JUMLA** | **17,072,042** | **4,196,100** | **6,223,131** | **162,289** | **1,500,000** | **555,000** | **4,354,200** | **81,321** | **6,490,521** |

Chanzo: WMJJWW, 2024/25

**Kiambatanisho Nam. 3: Makaazi ya Wazee Unguja na Pemba**

| Kituo | Idadi ya Wazee | | Jumla |
|---|---|---|---|
| | KE | ME | |
| 1. Sebleni | 13 | 06 | 19 |
| 2. Welezo | 13 | 28 | 41 |
| 3. Limbani (Pemba) | 02 | 05 | 07 |
| **JUMLA** | **28** | **39** | **67** |

Chanzo: WMJJWW, 2024/25

**Kiambatanisho Nam. 4: Taarifa ya Wazee walio katika Mpango wa Pencheni Jamii**

| Wilaya | ME | KE | Jumla | Wapya | Waliofariki |
|---|---|---|---|---|---|
| Kaskazini "A" | 1,507 | 2,242 | 3,749 | 205 | 85 |
| Kaskazini "B" | 744 | 1,058 | 1,802 | 205 | 64 |
| Kati | 938 | 1,071 | 2,005 | 204 | 53 |
| Kusini | 504 | 747 | 1,251 | 140 | 23 |
| Magharibi "A" | 884 | 1,161 | 2,045 | 266 | 84 |
| Magharibi "B" | 1,211 | 1,462 | 2,673 | 262 | 75 |
| Mjini | 2,608 | 2,997 | 5,615 | 521 | 256 |
| **Jumla Unguja** | **8,395** | **10,735** | **19,130** | **1,803** | **640** |
| Mkoani | 1,289 | 1,737 | 3,026 | 293 | 59 |
| Chakechake | 1,364 | 1,811 | 3,175 | 215 | 119 |
| Wete | 1,640 | 2,395 | 4,035 | 366 | 120 |
| Micheweni | 1,154 | 1,576 | 2,730 | 206 | 83 |
| **Jumla Pemba** | **5,447** | **7,519** | **12,966** | **1,080** | **381** |
| **Jumla Kuu** | **13,842** | **18,254** | **32,096** | **2,883** | **1,021** |

Chanzo: WMJJWW, 2024/2

**Kiambatanisho Nam. 5: Malalamiko ya Matunzo na Mvutano wa Malezi**

| Aina ya Malalmiko/Zanzibar | Yaliyoripotiwa | | Yaliyopatiwa ufumbuzi | | Yaliyopelekwa Rufaa | | Yanayoendelea na Usuluhishi | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | U | P | U | P | U | P | U | P |
| Matunzo | 214 | 40 | 127 | 33 | 50 | 01 | 37 | 06 |
| Mvutano wa Malezi | 147 | 20 | 87 | 17 | 41 | 03 | 19 | 00 |
| **Jumla** | **361** | **60** | **214** | **50** | **91** | **04** | **56** | **06** |

Chanzo: WMJJWW, 2024/25

**Kiambatanisho Nam. 6: Wahanga waliopo Nyumba Salama**

| Sababu za Kupokewa Kwenye Nyumba | Jinsia | | Umri | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| | KE | ME | | |
| Usafirishaji Haramu | 04 | 01 | 09-17 | 05 |
| Ndoa za umri mdogo | 01 | 00 | 16 | 01 |
| Kuzurura/Omba Omba | 01 | 00 | 16 | 01 |
| Kutelekezwa | 02 | 02 | 1-9 | 04 |
| Kupigwa | 01 | 01 | 8-13 | 02 |
| Kutoroka | 01 | 02 | 9-14 | 03 |
| Kudhalilishwa kingono | 03 | 03 | 9-17 | 06 |
| Kukizana na sheria | 00 | 01 | 12 | 01 |
| **Jumla kuu** | **13** | **10** | **1-17** | **23** |

Chanzo: Machi WMJJWW, 2024/25

**Kiambatanisho Nam. 7: Makosa yaliyopelekea watoto kupokewa katika Kituo cha Marekebisho ya Tabia**

| AINA YA MAKOSA | ME | KE | Jumla |
|---|---|---|---|
| Kukashifu | 01 | 00 | 01 |
| Kutoroka nyumbani | 08 | 01 | 09 |
| Kubaka | 01 | 00 | 01 |
| Mazingira hatarishi | 02 | 01 | 03 |
| **Jumla** | **12** | **02** | **14** |

Chanzo: Machi WMJJWW, 2024/25

**Kiambatanisho Nam. 8: Vituo Vya Kulelea Watoto Yatima**

| **Jina la Kituo** | **Ke** | **Me** | **Idadi ya Watoto** |
|---|---|---|---|
| Mazizini | 08 | 18 | 26 |
| Fatma House | 20 | 27 | 47 |
| Kidundo Orphanage Center | 10 | 14 | 24 |
| S.O.S | 12 | 08 | 20 |
| Darul - Ahbaab - Pemba | 00 | 45 | 45 |
| Sakina Girls | 19 | 00 | 19 |
| Salim Turkey Foundation | 34 | 00 | 34 |
| Assalam Orphanage Center | 09 | 16 | 25 |
| Zaso Children's Home | 22 | 27 | 49 |
| Al- Maftuh Foundation | 24 | 21 | 45 |
| Amani Foundation | 07 | 13 | 20 |
| Al- Nassir Foundation | 18 | 00 | 18 |
| Markaz Yaqeen | 34 | 00 | 34 |
| Rahmtu Al Khair Orphanage Centre | 00 | 92 | 92 |
| Maftuh Foundation | 16 | 14 | 30 |
| Montesori Orphange Centre | 11 | 09 | 20 |
| Jumla | **244** | **304** | **548** |

Chanzo: WMJJWW 2024/25

**Kiambatanisho Nam. 9: Vituo vya Malezi na Makuzi ya Awali ya Mtoto**

| Wilaya | Majina ya Vituo | Jumla | Idadi | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| **Unguja** | | | **Ke** | **Me** | |
| Mjini | Beautiful Mind Day Care and KG | 08 | 20 | 17 | 37 |
| | London Bridge | | 12 | 15 | 27 |
| | Itaqillah | | 05 | 08 | 13 |
| | Lale Bustani | | 09 | 11 | 20 |
| | Iqra Integrated Academy | | 05 | 08 | 13 |
| | Glorious Academy | | 42 | 49 | 91 |
| | Royal Children Centre | | 11 | 23 | 34 |
| | Sweet Baby Care | | 23 | 19 | 42 |
| Magharibi A | Brilliant Academy | 02 | 54 | 44 | 98 |
| | Blue Bird | | 22 | 18 | 40 |
| Magharibi B | Kids Space | 09 | 02 | 07 | 09 |
| | High Achievement | | 13 | 10 | 23 |
| | Laureate International School | | 40 | 56 | 96 |
| | Al Jawaher | | 22 | 23 | 45 |
| | First Step Day Care | | 29 | 15 | 44 |
| | High View School of Zanzibar | | 41 | 37 | 78 |
| | The Nest Day Care | | 10 | 16 | 26 |
| | Bright Star Day Care Centre | | 05 | 03 | 08 |
| | Amfar Baby Care | | 06 | 01 | 07 |
| Kaskazini B | Amici Marafiki | 01 | 63 | 66 | 39 |
| Kati | Semta Baby Care | 01 | 12 | 08 | 20 |
| Kusini | Kituo cha Malezi | 01 | 18 | 17 | 35 |
| **Jumla** | | **22** | **314** | **283** | **597** |
| **Pemba** | | | | | |
| Wete | Maandalizi Kamaria | 4 | - | 26 | 26 |
| | Rash-Ahmed Victory | | 26 | - | - |
| | Genius Kids Nursery | | 03 | 03 | 06 |
| | Best View Nursery | | 03 | 12 | 15 |
| | Istiqama – Wete Islamic | | 05 | 10 | 15 |
| Chake | Maktaba Nursery | 3 | 20 | 15 | 35 |

| Wilaya | Majina ya Vituo | Jumla | Idadi | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| **Unguja** | | | **Ke** | **Me** | |
| chake | Better Change | | 07 | 03 | 10 |
| | Alite Madungu Nursery | | 12 | 08 | 20 |
| Mkoani | Atlas | 3 | 06 | 09 | 15 |
| | New Mission Nursery | | 08 | 12 | 20 |
| | Mkanyageni Day Care Centre | | 15 | 08 | 23 |
| **Jumla** | | **10** | **132** | **124** | **256** |
| **Jumla Kuu** | | **32** | **446** | **407** | **853** |

Chanzo: WMJJWW 2024/2

**Kiambatanisho 10a: Idadi ya wafanyakazi kwa mujibu wa elimu zao**

| Kiwango cha elimu | Jinsi | | Jumla |
|---|---|---|---|
| | Me | Ke | |
| Shahada ya uzamivu | 01 | 00 | 01 |
| Shahada ya uzamili | 16 | 11 | 27 |
| Shahada ya kwanza | 24 | 56 | 80 |
| Postgraduate | 00 | 01 | 01 |
| Diploma | 07 | 20 | 27 |
| Cheti | 06 | 20 | 26 |
| Kidato cha sita | 01 | 03 | 04 |
| Kidato cha nne (iv) | 19 | 31 | 50 |
| Jumla | 115 | 199 | 314 |

Chanzo: WMJJWW 2024/25

**Kiambatanisho Nam 10b: Watumishi waliopo masomoni kwa muda mrefu**

| Aina ya masomo | Jinsi | | Jumla |
|---|---|---|---|
| | Me | Ke | |
| Gender and development | 01 | 00 | 01 |
| Social work | 02 | 02 | 04 |
| Economics | 00 | 01 | 01 |
| Computer science and technology | 01 | 00 | 01 |
| Management finance and accounting | 01 | 00 | 01 |
| Human resource management | 01 | 01 | 02 |
| Counselling and psychology | 00 | 03 | 03 |
| Social economy | 00 | 01 | 01 |
| Record and archive management | 00 | 01 | 01 |
| Community economic development | 01 | 00 | 01 |
| Jumla | 07 | 09 | 16 |

Chanzo: WMJJWW 2024/25

**Kiambatanisho Nam 10c: Watumishi waliopo masomoni kwa muda mfupi**

| Aina ya masomo | Jinsi | | Jumla |
|---|---|---|---|
| | Me | Ke | |
| Udereva | 04 | 00 | 04 |
| Ufungaji wa hesab na kodi | 10 | 00 | 01 |
| Green development and enviromental Protection for Africa countries | 00 | 01 | 01 |
| Umbukumbu na nyaraka | 02 | 01 | 03 |
| Poverty reduction and sustainable Delvopmentfor belt and road countries | 00 | 06 | 06 |
| Habari uhusiano na mawasiliano | 00 | 01 | 01 |
| Mafunzo ya uandishi wa kiswahili | 00 | 01 | 01 |
| Matumizi sanifu na fasaha ya kiswahili | 00 | 01 | 01 |
| Cross – boarder e - commerce | 01 | 01 | 02 |
| Sayansi ya malezi | 05 | 02 | 07 |
| **Jumla** | **13** | **14** | **27** |

Chanzo: WMJJWW 2024/25

**Kiambatanisho Nam. 11: Idadi ya Vikundi na Wajasiriamali kwenye Majukwaa ya Wanawake**

| Mikoa | Idadi ya Vikundi | Walioshiriki | Idadi ya Majukwaa |
|---|---|---|---|
| **Kaskazini Unguja** | **1,362** | **10,169** | **78** |
| **Kusini Unguja** | **388** | **7,500** | **66** |
| **Kaskazini Pemba** | **848** | **13,429** | **64** |
| **Kusini Pemba** | **973** | **8,300** | **71** |
| Jumla | 3,571 | 39,398 | 279 |

Chanzo: WMJJWW 2024/25

**Kiambatanisho Nam. 12: Maelezo ya Wizara kwenye bajeti inayozingatia usawa na jinsia**

Wizara ina wajibu wa kusimamia na kukuza usawa wa kijinsia, kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji kwa wanawake na watoto, kuwawezesha wanawake, kuimarisha maendeleo ya jamii na kutoa huduma pamoja na Kuhakikisha usimamizi wa Bajeti inayozingatia Usawa wa Kijinsia. Wajibu huo unalenga kuondosha vikwazo mbalimbali vinavyopelekea mchango mdogo katika uchumi wa nchi.

Uzoefu unaonesha kuwa nchi zilizoimarika kiuchumi zimekuwa zikitoa msukumo na mchango mkubwa katika kuzingatia jinsia ambapo wanahakikisha uwiano mkubwa baina ya wanawake na wanaume katika ngazi za maamuzi, wanabuni na kutekeleza mikakati maalum ya kuwawezesha wanawake kushiriki katika shughuli za kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Kwa mujibu wa Sensa ya Mwaka 2022 Idadi ya watu Zanzibar ni 1,889,773 (wanawake 974,281 na wanaume 915,492), sawa na ongezeko la idadi hiyo lilifikia asilimia 3.7. Ongezeko la ukuaji wa idadi ya watu linahusishwa na kiwango cha hali ya juu cha utegemezi, hali ya mahitaji ya msingi na chakula, ushiriki mdogo wa wanawake kwenye nguvukazi na kuongezeka kwa matumizi ya rasilimali kuliko uwezo wake.

Changamoto kwa Zanzibar ni kufanikisha malengo ya kupunguza umasikini yaliyoainishwa katika Dira ya 2050 (kiwango cha umasikini wa mahitaji ya msingi cha asilimia 20.6 na kiwango cha umasikini wa chakula cha asilimia 7) ifikapo 2030.

Ushiriki wa wanawake katika nguvu kazi ulikuwa juu kwa 80% mnamo mwaka 2019. SIGI Tanzania ripoti imeeleza kuwa asilimia 63 ya wanawake wa umri wa kufanya kazi wako katika nguvu kazi, na asilimia 58 wameajiriwa, ikilinganishwa na asilimia 75 na 69 ya wanaume. Tofauti zinajidhihirisha zaidi Zanzibar ambako pengo la kijinsia katika ushiriki wa nguvu kazi linafikia alama 20 za asilimia, na pengo la ajira linasimama kwenye alama 28 za asilimia. Hivyo, uwezeshaji wa kiuchumi wa wanawake unajumuisha masuala mbalimbali, hasa udhibiti wa muda wao, maisha yao, na miili yao, pamoja na ushiriki wenye maana na uwakilishi katika michakato ya maamuzi ya kiuchumi katika ngazi zote—kuanzia ndani ya kaya hadi nafasi za juu za kiuchumi na kisiasa (UNWOMEN, 2020).

Idadi ya wanawake walioingia katika uongozi kupitia uchaguzi mkuu walifikia 29 sawa na asilimia 37; Mawaziri 6 sawa na asilimia 33; Naibu Waziri 3 sawa na asilimia 43. Takwimu za Viongozi wengine katika Utumishi wa Umma zinaonesha kuwa Makatibu wakuu 10 sawa na asilimia 38; Manaibu Katibu Wakuu 5 sawa na asilimia 28; Wakurugenzi/Makamishna 44 sawa na asilimia 24. Aidha, viongozi katika Mfumo wa Mahakama wanahusisha Majaji 5 sawa na asilimia 36; na Mahakimu 23 sawa na asilimia 35.

Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imepangwa kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kufanya uchambuzi katika ngazi zote za kiutumishi kwa kuzingatia uwiano wa kijinsia;

ii. Kupunguza matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia

iii. Kuengeza nafasi za ushiriki wa wanawake katika nafasi za maamuzi/uongozi

iv. Kuongeza idadi ya wajasiriamali wanawake kwa kuwaunganisha na fursa mbalimbali ikiwemo mikopo na masoko;

v. Kuhamasisha jamii kuwa na familia bora na malezi bora kwa watoto;

vi. Kupunguza hali na uhatarishi wa mazingira magumu kwa kuwezesha familia zilizo chini ya kiwango cha umasikini kiuchumi; na

vii. Kuwawezesha wanaume kushiriki katika jitihada za kuwaendeleza wanawake kwa maslahi ya taifa, ikiwa ni pamoja na kutekeleza Programu ya Wanaume wa Mabadiliko (Male Champion)

Aidha, kwa mwaka wa Fedha 2025/2026 Wizara inatarajia kuendeleza utekelezaji wa Bajeti yenye mtazamo wa kijinsia jumla ya shilingi **3,587,487,624** zimepangiwa kutekelezwa kwa mwaka huu.